

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

Simu: 023 2010199

Kipepesi: 023 20111338

Barua pepe:mafiaadc@pwani.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
P. O Box 85
MAFIA.

Kumb Na. MDC/S.20/5/VOL.II/45

05 Septemba, 2017

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya Mafia imepata kibali cha Ajira kutoka kwa katibu Mkuu Ofisi ya Raisi Menejimenti ya utumishi wa umma kupitia Barua yenyé Kumb Na. FA 170/375/01/47 ya tarehe 31 Julai, 2017. Kupitia barua hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa kuomba ili kujaza nafasi wazi.

1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III- TGS B (NAFASI 2)

1.1 SIFA ZA MWOMBANJI:

Mwombaji awe ni mwenye ufaulu wa Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliye hitimu mafunzo ya Astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka chuo cha serikari za mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na serikali

1.2 MSHAHARA.

Kwa kuzingatia viwango vya Mishahara yaani **TGS B1**

1.3 KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIJI

- i. Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Kijiji
- ii. Kusimamia ulinzi na usalama wa Raia na mali zao. Kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji

- iv. Katibu wa Mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera , Sheria na Taratibu
- vi. Kujibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa umasikini,Njaa na kuongeza uazalishaji wa mali
- vii. Kiongozi wa wakuu wa vitengo katika Kijiji
- viii. Kuibua vyanzo vya Mapato na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Kijiji
- ix. Kuandaa na kutunza Rejestra ya wakazi wote wa Kijiji
- x. Atawajibika kwa mtendaji wa kata na Mkurugenzi Mtendaji.

1.4 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45
- ii. Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- iii. Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi yanayo jitoshaleza (detailed CV) yenye anuani na namba za simu pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu(3) wa kuaminika
- iv. Maombi yote yaambatane na barua ya maombi . nakala ya vyeti vya taaluma, nakala ya vyeti vya kidato cha Nne au Sita kwa walio fikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- v. Waombaji waambatanishe picha mbili za passport size za hivi karibuni
- vi. Testimonials , Provisional results, statement of results, hati ya matokeo ya kidato cha Nne na Sita havita kubaliwa

- vii. **Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 16 Septemba 2017**

Maombi yote yawasilishwe masijala kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) au kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (w)
Halmashauri ya Wilaya Mafia
S.L.P 85
MAFIA

Imetolewa na



.....
ERICK C. MAPUNDA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MAFIA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

S. L. P. 85

MAFIA - D. C.